# KANUNI *za* KILIMO HAI

# UTANGULIZI

Kanuni hizi ndiyo msingi ambao kilimo hai huchipukia na kukua, zinawasilisha mchango ambao kilimo hai kinaweza kutoa duniani na kuwepo dira ya kuboresha kilimo ulimwenguni kwa ujumla wake.

Kilimo ni moja ya shughuli muhimu sana kwa binadamu, kwa kuwa kila mtu anahitaji kujikimu kila siku. Historia, mila na amali za watu katika jamii zinaambatana na kilimo. Kanuni hizi zinahusisha mtazamo wa watu kuhusu udongo, maji, mimea na wanyama katika kuzalisha, kuandaa na kusambaza chakula na bidhaa nyingine. Zinaweka mkazo katika ardhi, mahusiano ya kimaumbile na kuweka dira ya matumaini kwa vizazi vijavyo.

Kanuni za kilimo hai zinalenga kuhuisha vuguvugu la kilimo hai katika nyanja zote na kutoa mwongozo kwa "IFOAM" katika kuweka vipaumbele vya mipango ya maendeleo, viwango na kuwasilisha mtazamo wa kilimohai kuhusu ulimwengu.







## Kilimo Hai

kimejikita katika kanuni nne za msingi: **Kanuni ya Afya**

**Kanuni ya Mazingira**

**Kanuni ya Haki na Usawa**

**Kanuni ya Uangalizi**

Kila moja ya kanuni hizi ina kauli mbiu inayofuatiwa na maelezo ya ufafanuzi. Kanuni hizi zinatumika na kuangaliwa kwa ujumla wake na kuwa mfumo kamili. Zimewekwa kuwa kanuni zinazosimamia maadili yanayo hamasisha uwajibikaji kwa ulimwengu.

# ***Kanuni*** *ya* AFYA

Kilimo hai sharti kiwe endelevu kwa kuzingatia urutubishaji udongo na kuboresha afya ya mimea, wanyama na binadamu katika sayari ya dunia bila utengano wa aina yoyote.



Kanuni hii inaonyesha kwamba afya ya watu au jamii ni jambo lisiloweza kutenganishwa na mfumo wa kimazingira. Ardhi yenye rutuba huzalisha mazao bora kwa afya ya binadamu na wanyama.

Afya ni mfumo wa uhai na utaratibu wa maisha kwa ujumla unaozingatia siyo tu kutokuwepo kwa magonjwa bali kuujali na kuutunza mwili, akili, ustawi wa jamii na mazingira bora na mazuri ya kuishi. Uwezo wa kujikinga, kushiriki na kuendeleza uumbaji pamoja na kujijali ni tabia za msingi na muhimu kwa afya bora.

Jukumu la kilimo hai katika ulimaji, usindikaji, usambazaji au ulaji huambatana na uendelezaji na uboreshaji wa afya na uhai wa mfumo wa mazingira na viumbe wa aina zote kuanzia kwenye udongo hadi kwa binadamu. Pia kilimo hai kinalenga katika uzalishaji wa chakula chenye viwango vya ubora na usalama wa hali ya juu ili kuchangia katika kujikinga na kujenga siha nzuri. Kwa mtazamo huu kanuni za kilimo hai zinapaswa kuzuia matumizi ya mbolea, madawa ya wadudu au magonjwa ya mifugo na viuatilifu au vinasaba vinavyoongezwa katika hifadhi ya vyakula ambavyo vinaweza kusababisha madhara ya kiafya kwa mlaji au mtumiaji.

# ***Kanuni*** *ya* MAZINGIRA

Kilimo hai kinasimamia na kujali uhai wa mfumo wa mazingira na mzunguko wa asili, kuishi na kufanya kazi sanjari na kuyafanya kuwa endelevu.



Kanuni hii inawezesha kilimo hai kuhuisha na kuhifadhi mazingira. Inaweka mkazo katika uzalishaji unaolenga na kutegemea mfumo endelevu wa kimazingira. Hali bora na ustawi hupatikana kutokana na mazingira ya uzalishaji yanayojali uhai wa viumbe wengine. Kwa mfano, uzalishaji wa mazao unapaswa kuzingatia na kujali urutubishaji wa udongo, ufugaji wanyama unaozingatia mfumo wa kimazingira wa shamba, ufugaji wa samaki na viumbe hai wa baharini uzingatie mfumo wa mazingira ya bahari.

Ufugaji na utaratibu wa mavuno ya mazao ya msituni yafaa uendane na mzunguko wa kiikolojia na uwiano asili wa kimazingira. Kilimo hai lazima kiendana na mazingira ya kawaida na utamaduni wa mahali husika. Inasisitizwa kuwa matumizi ya malighafi au pembejeo uzingatie hali ya kuweza kurudiwa na kutumiwa au kurejeshwa upya. Usimamizi sahihi wa malighafi, vifaa na nishati unahuisha na kuboresha mazingira kwa kuhifadhi maliasili na rasilimali.

Kilimo hai kinaweka uwiano wa kimazingira kwa kubuni na kuhimiza mfumo wa uzalishaji unaoweka mazingira bora kwa makazi na kutunza urithi wa kimaumbile na kilimo. Wazalishaji, Wasindikaji, Wauzaji au Watumiaji wa bidhaa za kilimo hai wanapaswa kuyalinda na kuyatunza mazingira kwa ujumla wake pamoja na hali ya hewa, viumbe, bioanuai, hewa na maji.

# *Kanuni ya*
# HAKI na USAWA

Kilimo hai kinajenga mahusiano yanayohakikisha utoaji wa haki katika mazingira na fursa za maisha.



Haki inayojali na kuzingatia usawa, heshima, na usimamizi wa ulimwengu kwa pamoja na kukuza mahusiano ya viumbe hai.


Kanuni hii inasisitiza kwamba, wale wote wanaojihusisha na kilimo hai ni lazima wazingatie mahusiano yenye usawa katika ngazi zote bila upendeleo, iwe ni wazalishaji, walaji, wasindikaji, wafanyakazi, wafanyabiashara au wasambazaji ili kuhuisha na kuboresha mazingira na kuhifadhi maliasili na rasilimali. Kilimo hai lazima kilete uwiano na urari wa kimazingira kwa kubuni na kuhimiza mfumo wa uzalishaji unaoweka mazingira bora kwa makazi na kutunza rasilimali katika jitihada za kuendeleza kilimo. Wazalishaji, wasindikaji, wauzaji au wanunuzi, walaji na watumiaji wote wa bidhaa za kilimo hai wanapaswa kushiriki kikamilifu katika kukinga na kuzuia uharibifu wa mfumo mzima wa mazingira unaojumuisha mandhari, viumbe, bionuai, hewa na maji.

Kilimo hai kinapaswa kuwapatia maisha bora na mazuri wale wote wanaojihusisha na mfumo huu wa uzalishaji na kuchangia katika uhakika wa chakula na kupunguza umaskini. Kilimo hai kinalenga katika kuzalisha chakula na bidhaa za kutosha kwa kuzingatia viwango vya ubora na usalama.

Kanuni hii inasisitiza kwamba wanyama lazima wapatiwe fursa na hali ya kimazingira inayoendana na maumbile, tabia na ustawi wao. Rasilimali na maliasili zilizopo katika mazingira ambazo hutumika katika uzalishaji au matumizi mengine ni lazima zisimamiwe vema na matumizi hayo yalete tija kwa jamii na ikolojia ambayo ni haki na urithi wa vizazi vijavyo. Haki inahitaji mfumo wa uzalishaji, usambazaji na biashara ulio wazi na unaotoa usawa na uwajibikaji katika kuleta mazingira ya maisha bora kwa jamii.

# *Kanuni ya*
# UANGALIZI

Kilimo hai kinatoa tahadhari na uwajibikaji unaoweka kinga kwa afya na ustawi wa vizazi vya sasa na vijavyo pamoja na kujali mazingira endelevu.



Mfumo wa kilimo hai unayosifa ya kubadilika ili kuendana na matakwa ya hali ya ndani au nje ya mazingira husika. Wanaojihusisha na kilimo hiki wanapaswa kuongeza ufanisi na uzalishaji wenye tija, bila kuathiri afya na ustawi wa wahusika au viumbe. Hivyo, teknolojia mpya zinapaswa kufanyiwa tathimini yakinifu na mbinu zilizopo (za asili) zifanyiwe utafiti wa kina. Hili linatokana hasa na kutoeleweka kinaga ubaga kwa mahusiano sawia ya mfumo wa kimazingira na kilimo, kwa hiyo tahadhari ya Uangalizi lazima ichukuliwe.

Kanuni hii inasema kwamba tahadhari na uwajibikaji ni masuala muhimu sana katika kusimamia, kuendeleza na kuchagua teknolojia za kilimo hai. Sayansi ni muhimu katika kuhakikisha kwamba kilimo hai ni mfumo sahihi kiafya, kiusalama na kimazingira. Hata hivyo, maarifa ya kisayansi pekee hayatoshi. Bali uzoefu wa kiutendaji, hekima, busara na ubunifu uliojengeka kwa miongo kadhaa husaidia katika kutatua matatizo ya aina mbalimbali ya kuizalishaji na maendelezo. Kilimo hai lazima kizuie athari za wazi zinazoweza kujitokeza kwa kubuni na kutumia teknolojia sahihi. Pia kukataa teknolojia zisizokuwa endelevu ambazo athari zake hazijafahamika bayana kama vile ya viini tete (GMO). Maamuzi lazima yazingatie amali na mahitaji ya wote wanaoweza kuathirika, kwa kutumia mchakato ulio wazi wa ushirikishwaji jamii.

This document is a translation of the English document entitled "Principles of Organic Agriculture", which text was adopted by the IFOAM General assembly in Adelaide in 2005 and is the only official reference for the Principles. IFOAM does not endorse responsibility for the content of this translated version. For any doubt regarding the exact meaning of its content, please refer to the English version.





IFOAM's mission is leading, uniting and assisting the organic movement in its full diversity.

Our goal is the worldwide adoption of ecologically, socially and economically sound systems that are based on the principles of organic agriculture.

**IFOAM HEAD OFFICE**
Charles-de-Gaulle-Str. 5
53113 Bonn, Germany
Phone: +49 - 228 - 92650 - 10
Fax: +49 - 228 - 92650 - 99
Email: HeadOffice@ifoam.bio
www.ifoam.bio